



CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

NAFASI YA KAZI

Chama cha Walimu Tanzania ni Chama cha Wafanyakazi kutoka kada ya Walimu ambacho shughuli zake zipo Tanzania Bara tu. Chama kimesajiliwa kwa Namba 004 chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004 na kinaajiri Wafanyakazi kwa ajira ya kudumu ambao wapo katika kila Mikoa, Wilaya na Makao Makuu. Ili kuboresha huduma kwa wanachama, CWT kinatangaza nafasi za ajira ya Katibu Muhtasi na Mwanasheria kwa Mtanzania yeyote mwenye sifa ambaye atakuwa tayari kufanya kazi mahala popote Tanzania.

1. KATIBU MUHTASI - NAFASI 02

Sifa za waombaji

Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

- Awe amehitimu kidato cha nne au zaidi.
- Awe na Cheti (NTA LEVEL 5) au Stashahada au Diploma ya U hazili inayotambuliwa na NACTE.
- Awe na uzoefu wa kutumia kompyuta na matumizi ya intaneti
- Awe na uzoefu usiopungua miaka miwili.
- Awe na uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha.

Majukumu ya kazi:

- Kupiga chapa nyaraka mbalimbali za Chama.
- Kutunza kumbukumbu mbalimbali kama atakavyoelekezwa na mkuu wake wa kazi.
- Kupokea wageni na kuwaelekeza mahali wanapoweza kusaidiwa
- Kupokea mawasiliano mbalimbali ya ofisi na kumpatia msimamizi wa kazi
- Kufanya usafi ofisi za chama
- Kutunza siri zote za ofisi na kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wa kazi.

NB: Makatibu Muhtasi walioitwa kwenye usaili tarehe **06 Mei 2022** kupitia gazeti la tarehe **29 Aprili 2022** wasiombe kwani tangazo hili haliwahusu.

MWANASHERIA –NAFASI 02

Sifa za mwombaji

- Awe na Shahada ya Kwanza ya Sheria (LLB) kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.
- Awe na uwezo wa kuongea kwa ufasaha na kuandika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta.
- Awe na uzoefu usiopungua miaka miwili.
- Awe raia wa Tanzania.

Majukumu ya kazi

- Kutoa ushauri wa Kisheria kwa Walimu na Chama.
- Kutatua migogoro ya kikazi wanayokabiliana nayo Walimu.
- Kufuatilia suluhu ya maatizo mbalimbali ya Walimu katika ofisi mbalimbali za Serikali na Waajiri.
- Kuandaa taarifa ya kazi za Idara za robo mwaka, nusu mwaka na Mwaka mzima.
- Kuandaa bajeti ya Idara.
- Kuhakikisha Idara inapata makala mbalimbali za Kisheria.
- Kufuatilia na kupata mabadiliko mbalimbali ya Sheria (Amendments) pamoja na Gazeti la Serikali (Government Gazette).
- Kufuatilia upatikanaji wa hukumu za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa (Authorities).
- Kutunza Maktaba ya mambo ya Sheria.
- Kufanya kazi nyingine atakazotumwa na Katibu Mkuu au Mkuu wa Idara.

MASHARTI YA JUMLA

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Viambatisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.
- Cheti cha mtihamu wa Kidato cha IV na VI.
- Vyeti vya kitaaluma.
- Waombaji wawe na uzoefu usiopungua miaka miwili.
- Picha moja 'passport size' ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
- Waombaji watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23 Juni, 2022 saa 10.00 Jioni kupitia anuani ifuatayo:-

Katibu Mkuu,
Chama cha Walimu Tanzania, S.L.P. 3077, DODOMA.
Barua pepe: info@ttu.or.tz

Imetolewa na:


Mwl. Deus G. Seif
KATIBU MKUU - CWT

KATIBU MKUU
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
MAKAO MAKUU - DODOMA

ORD00007644